




**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MTWARA  
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)**



Simu: 023-2333928  
Barua pepe: dedmtwara@mtwaradc.go.tz

S.L.P. 528,  
**MTWARA.**

**Unapojibu tafadhali taja:**

Kumb. Na **AC.341/695/01/45**

16/09/2024

**TANGAZO**

Msimamizi wa Uchaguzi wa Halmashauri ya Wilaya Mtwara anawatangazia Watumishi wote wa Umma nafasi za kazi za muda mfupi kwa ajili ya shughuli za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika tarehe 27 Novemba 2024.

1. Nafasi zinazotangazwa
  - i. Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya Kituo
  - ii. Afisa Mwandikishaji wa Wapiga kura
2. Sifa zinazotakiwa
  - i. Asiwe na dhamana au uongozi katika chama chochote cha siasa
  - ii. Awe ni Mtumishi katika Utumishi wa Umma (Public Service)
  - iii. Awe mwadilifu
3. Maelekezo ya jumla
  - i. Barua zote ziandikwe kwa mkono
  - ii. Barua iandikwe majina kamili yanayotumika katika Utumishi
  - iii. Barua itaje nafasi ya kazi unayoomba
  - iv. Barua itaje cheo katika Utumishi wa Umma
  - v. Barua itaje kituo cha kazi
  - vi. Barua iwe na anuani kamili ikiwa na namba ya simu inayopatikana wakati wote
  - vii. Barua iambatishwe na maelezo binafsi (CV)
  - viii. Barua ziwasilishwe kwa mkono masijala ya wazi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) Mtwara
  - ix. Watendaji wa Kata na Vijiji hawaruhusiwi kuomba nafasi hizi za kazi
  - x. Barua ziandikwe kwa;  
Msimamizi wa Uchaguzi,

Jimbo la Mtwara Vijijini,  
S.L.P 528,  
**MTWARA.**

4. Mwisho wa kupokea maombi hayo ni tarehe 20/09/2024

Tangazo hili limetolewa na;

Abeid A. Kafunda  
**MSIMAMIZI WA UCHAGUZI**  
**JIMBO LA MTWARA VIJIJINI**